**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MACHAME**

**Namba za simu**
**Mkuu wa Shule** 0754349771/0658349771 S. L. P 3043
**Makamu M/Shule** 0621069632/0713621278 MOSHI
**Matron** 0768516526/0769796407/0652115322 11/05/2018

**Mzazi/ mlezi wa wanafunzi** …………………………………………………S.L.P ………..…

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MACHAME HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI MKOA KILIMANJARO MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2018/2019** Tahasusi ya ……………… Shule ya Sekondari ya Wasichana MACHAME ipo umbali wa **kilometa 25** Magharibi mwa mji wa Moshi. Usafiri wa basi kutoka Moshi mjini unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi Moshi mjini. Nauli ni shilingi **1,000/= tu.** Muhula wa masomo unaanza **.../07/2018**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **.../07/2018.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **..............**
2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 **Sare ya shule**

**A. Sare ya shule hii ni**

i. Sketi 02 rangi ya kijani iliyokolea (maelezo ya mshono angalia kiambatanisho nyuma)
ii. Mashati 02 meupe ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya hijab (kijuba – kwa waislam tu) ni nyeupe isiwe na urembo wowote isipokuwa lesi chini (Angalia kiambatanisho nyuma)
iv. T- Shirt nzito ya rangi ya kijivu.
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba kuanzia matundu 03 vyenye visigino vifupi (visiwe simpo fashion)
vi. Soksi jozi nne ndefu nyeupe
vii. Sweta 02 za kijani ( Zisiwe na rangi ingine yoyote )
   - Sweta 01 iwe ya mikono mirefu
   - Sweta ingine iwe ya mikono mifupi (Kizibao) (Angalia kiambatanisho nyuma).
viii. Tai moja ya Kijani (Ishonwe kutokana na kitambaa cha Sketi)
ix. Pull neck nyeupe (Kabashingo)
x. Rain Boot na mwavuli.

**B. Sare za Michezo kwa shule hii ni:-**

i. Track suit 01 – rangi ya kijani yenye mistari meupe pembeni na isiyobana chini.
ii. T- Shirt nyeupe 02 (Zisizo na maandishi yoyote)
iii. Raba/viatu vya michezo - rangi yoyote

**C. Nguo za kushindia (Shamba dress)**

i. Magauni mawili ya kijani draft (checked material) urefu wake kwenye magoti ( Angalia kiambatanisho)
ii. Suruali mbili nyeusi za kitambaa (Jeans/skin tight/suruali za kubana haziruhusiwi)
iii. Sweta mbili nyeusi zenye kofia zisizo na urembo wala maandishi yoyote(zinapatikana kwenye mitumba pia).

**2.2 Ada na Michango ya shule**

A. Ada ya shuule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa mhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye **Akaunti ya shule Na. 40101200068 katika Benki ya NMB –Machame Girls' Sec. School Recurrent Account.**( Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

B. **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
vi. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na Bima ya Afya Tshs. 50,400/= (wanafunzi wanashauriwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya NHIF kwa wale tu wasiokuwa na Bima ya Afya)
vii. Shilingi 10,000/= kukodisha godoro kwa muhula (yanapatikana shuleni)
viii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

N.B: Michango yote ilipwe kwenye **Akaunti,ya shule Na. 40110006081 NMB – Machame Secondary School**

C. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Ream ya karatasi 1( $A_4$) Photocopy
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa)
iii. Dissecting kit kwa mwanafunziwa Biolojia
iv. Scientific calcutator – kwa masomo ya Sayansi na Hisabati
v. Mashuka pair 2 – pink , blanketi 1 zito, foronya 2- Pink, chandarua 1 – bluu na mto 1
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko, na kikombe) vyote vya bati
vii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko

**D. VIFAA VYA USAFI**

| NAMBA | AINA YA KIFAA | TAHASUSI |
|---|---|---|
| 1 | Kwanja & squeezer yenye mpini | HGL |
| 2 | Jembe na mpini | CBA |
| 3 | Reki & squeezer yenye mpini | HKL |
| 4 | Mifagio (chelewa) na Brashi za kusugulia choo | WOTE |
| 5 | Hard broom & panga | EGM |
| 6 | Hard broom & panga | CBG |
| 7 | Squeezer yenye mpini na panga | CBN |

E. **MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA**

1. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip).
2. Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne. (leaving certificate).
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (birth certificate).
4. Begi la kubeba vitabu na madaftari (pochi haziruhusiwi kamwe).
5. Counter books" 10 (quire three) kwa ajili ya masomo darasani.
6. Madaftari madogo 12 kwa ajili ya mazoezi ya kila siku darasani .
7. Kalamu za wino na penseli za kutosha.
8. Kufuli dogo imara la kufungia dawati/ kabati.

F. **VIAMBATANISHO MUHIMU**

Angalia viambatanisho vifuatavyo:-

1. Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi
2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
3. Sheria za shule
4. Fomu ya kukubali nafasi
5. Picha (4) za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
6. Michoro na mishono ya Sare za shule.
7. Orodha ya vitabu vya masomo

**NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MACHAME.**

Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………….

Jina la Mkuu wa Shule A. F. MASSAWE….

Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………….

*Machame Girls' Secondary School*
*P. O. Box 3043, Moshi.Mobile 0754349771. Fax 0272756897*

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the candidate)**

Surname………………………… Other names…………………….. ……………………………..

Age ……………… Sex…………… Combination……………… School……………………………

**PART II: PERSONAL HISTORY (To be filled by medically qualified and registered professional)**

Are you suffering of have you suffered from any of the following? Indicate **Yes** or **No**

1. Tuberculosis…………………………… Epilepsy………………………….
2. Asthma……………………............... Deformity……………………….
3. Rheumatic fever……………………… Mental illness………………….
4. Allergic disorders…………………… Eye disorder…………………….
5. Heart disease………………………….. Ear, Nose, Throat disorder……………
6. Gastric or duodenal ulcers………….. Skin disease……………………..
7. Jaundice ……………………………… Anemia………………………….
8. Dysentery…………………………… Varicose veins…………………
9. Kidney disease…………………….. Diabetes…………………………
10. Gynecological disorder………………. Any other serious disorder (specify)…………….

**PART III: PHISICAL EXAMINATION**

1. Height (cm) ……………………………...
2. Skin…………………………………………..
3. Weight (kg)……………………………….
4. Eyes: Conjunctive…………………….. Pupil……………… Vision

   Right……………………………………. Left………………..
5. Ears (state if any discharge)………………. Mouth/throat……………….
6. Nose…………………………… Respiratory system……………………………

7. Abdomen…………………….. Any abnormality………………………………..

8. Cardiovascular system………………. Blood pressure ………………………………..

   Systolic ……………………………………… Diastolic…………………………………

   Heart: Any murmur ………………………………. Arteries veins ……………………

**PART IV: LABORATORY**

1. Urine: Albumin…………………………… Sugar………………….
   Leucocytes…………………
   Schistosoma…………………. …………………………
2. Stool: Special emphasis on hookworms or schistosoma………………………………..

3. Blood examination

   a) Hb level…………………………………….
   b) Neutrophil………………………………….
   c) Eosinophils……………………………....
   d) Basophiles…………………………………..
   e) Lymphocytes………………………………..
   f) Monocytes…………………………………..
   g) ESR………………………………………

4. X – Ray examination: Chest (include Radiologist's report)………………………….
5. Serology Widal test …………………… VDRL……………………………………
6. Pregnancy test………………………….

**PART V: CONCLUSION**

I have examined Miss…………………………………… and consider that she is physically and mentally fit/not fit to be admitted for secondary education.

Name………………………………….. Title……………………..
Qualification………………………….. Signature…………………. Date………………..
Address………………………..
.....................................................
.....................................................

*Machame Girls' Secondary School*
*P. O. Box 3043, Moshi.Mobile 0754349771. Fax 0272756897*

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**HABARI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi ……………………… 2. Tarehe ya kuzaliwa ………………
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa ……………………….……. Wilaya …………………
Tarafa ……………………… Kata………………….. Kijiji/Mtaa …………
4. Dini …………..… 5. Dhehebu………………….….. Kabila ………………….

**HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la baba mzazi/mlezi………………………Anuani…………………….
Namba ya simu ya kiganjani………………. Simu ya Ofisini………………
Kazi ya baba mzazi/mlezi……………………………….. Yuko hai?
Ndiyo/Hapana (Kata isiyohusika)
2. Jina la mama mzazi/mlezi……………………Anuani………...……………….
Namba ya simu ya kiganjani……………….. Simu yaOfisini……………
Kazi ya mama mzazi/mlezi………………….Yuko hai?

| Picha ya Baba Mzazi /Mlezi | Picha ya Mama Mzazi /Mlezi |
|---|---|

3 Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa za matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.

(I) Jina kamili …………………………………..Anuani……………………

Namba ya simu ya kiganjani ………………... Simu ya ofisini ……………
Kazi yake ……………………. Uhusiano na mwanafunzi …………………
(II) Jina kamili ……………………………………. Anuani ………………..

Namba ya simu ya kiganjani ……………. Simu ya ofisini ……………
Kazi yake ……………… uhusiano na mwanafunzi …………………

| (i) Picha ya Ndugu wa Karibu | (ii) Picha ya Ndugu wa Karibu |
|---|---|

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MACHAME**

# SHERIA ZA SHULE

Sheria na kanuni mbalimbali hutumika kama miongozo ya kumwezesha mwanadamu anayeishi katika jumuia yoyote kuwa na mahusiano mazuri na wenzake kwa kumwekea mipaka ya kiutendaji pamoja na kusimamia uhuru ambao ukizidi kiwango unaweza kuleta madhara. Aidha miongozo hii humwezesha mlengwa kukua na kuendelea kwa kuimarisha uhusiano mzuri wa kila siku katika jamii inayomzunguka. Sheria na kanuni za mahali au Taasisi hubuniwa na wanajamii wenyewe kulingana na malengo yao na mazingira yanayowazunguka ambapo kila mmoja hukubali kuzifuata bila kuacha. Sheria na kanuni huainisha bayana haki na wajibu wa kila mmoja katika jamii au Taasisi husika ili kuleta nidhamu na maendeleo ya pamoja. Hivyo kama kila mmoja katika jumuiya husika atazishika na kuzifuata sheria na kanuni zilizokubalika katika eneo lake kwa moyo mkunjufu, maisha huwa bora, yenye amani tele na furaha.

Kwa mtazamo huu, shule ya Sekondari ya Wasichana Machame inazo sheria rahisi sana zinazoelekeza haki na wajibu wa mwanafunzi atakayechaguliwa kujiunga na shule hii ili aweze kutimiza malengo yake ya kusoma na kufaulu na hatimaye akajenge familia na taifa lake. Adhabu ya ukiukwaji wa sheria hizi pia zinawekwa bayana ambapo mzazi na mwanafunzi wanatakiwa kuridhia.

## 1. HAKI ZA MWANAFUNZI

Mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana Machame anazo haki zifuatazo:

i. Kufundishwa masomo aliyochagua kwa idadi ya vipindi na muda ulioainishwa katika muhtasari wa kila somo.

ii. Kupewa majaribio, mazoezi na mitihani ya kumpima uelewa wake katika masomo aliyofundishwa kwa wakati kulingana na ratiba ya shule.

iii. Kuomba ufafanuzi kwa Mwalimu husika kwa kutumia taratibu zilizowekwa na shule kama hukupewa majaribio na mazoezi ya kutosha kulingana na taratibu za Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

iv. Kupatiwa mahali safi na salama pa kulala kwa muda wote awapo shuleni.

v. Kupata mlo wa kutosha kwa nyakati zote zinazotakiwa kama ilivyoainishwa katika ratiba ya shule.

vi. Kulindwa dhidi ya ajali wakati wote awapo shuleni.

vii. Kuadhibiwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake au kufuata sheria na taratibu za shule hii au za nchi.

2. **WAJIBU WA MWANAFUNZI**

i. Kujifunza kwa bidii na maarifa ili kufaulu masomo yote anayosoma kwa kiwango cha alama 65% na kuendelea.
ii. Kutii kwa moyo wa dhati sheria za nchi, za serikali za mitaa, kijiji pamoja na sheria za shule wakati wote awapo shuleni
iii. Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo katika mazingira ya shule na anaposafiri wakati wa likizo
iv. Kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote iliyoainishwa katika ratiba ya shule.
v. Kuhudhuria stadi ya usiku kila siku bila kukosa ili kujiandaa vyema na mitihani na majaribio yote ikiwemo mtihani wa taifa.
vi. Kutunza, kuheshimu na kuthamini mali za shule, mali za wenzake pamoja na mali zake mwenyewe kwa kuhakikisha kila kifaa mfano, madawati, meza, vifaa vya usafi n.k vimehifadhiwa mahali panapotakiwa na katika hali ya usafi.
vii. Kutii na kuitika mara asikiapo kengele inayomtaka afanye jambo Fulani lililoelekezwa katika ratiba ya shule
viii. Kupata milo yote ya chakula bila kukosa kwa kisingizio chochote kama siyo ugonjwa ambao umethibitishwa na daktari.
ix. Kuhudhuria masomo yote yafundishwayo darasani bila kukosa wala kuchelewa.
x. Kulinda na kufanya usafi wa mazingira ya shule kulingana na taratibu na mpangilio uliowekwa na shule na akae eneo lake hadi akaguliwe.
xi. Kutotupa taka ovyo, kuokota taka zilizotupwa hovyo na kuhifadhi katika pipa la taka katika eneo husika.
xii. Kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi wa baraza la wanafunzi bila ubishi wala manung'uniko na kufuata maelekezo yote yatolewayo na walimu pamoja na viongozi wa baraza la wanafunzi.
xiii. Kuhudhuria ibada na sala kwa muda uliopangwa na katika eneo husika kwa dhehebu lake kulingana na ratiba na taratibu za shule.
xiv. Kutunza na kuheshimu muda kwa kutembea haraka/kukimbia wakati wote anapoelekea eneo lolote ndani ya shule au nje ya shule
xv. Kutunza nishati ya umeme kwa kuzima taa baada ya kumaliza matumizi yake. Mf. Madarasani na mabwenini.
xvi. Kutunza maji kwa kutunza na kufunga bomba baada ya kumaliza matumizi yake.
xvii. Kufanya mazoezi kwa kukimbia mchakamchaka asubuhi kila siku za masomo bila kukosa kwa kisingizio chochote isipokuwa ugonjwa uliothibitishwa na daktari kwa ajili ya kuchangamsha mwili na akili.

3. **WAJIBU WA MZAZI**

Kila mzazi mwenye mwanafunzi katika shule ya Sekondari ya Wasichana Machame ana wajibu ufuatao kwa mwanaye na kwa shule:

i. Kulipa ada na michango yote kwa ajili ya masomo ya mwanaye kwa wakati na kwa kiwango kilichoainishwa katika barua ya kujiunga na shule na makala nyingine zinazotumwa kwa wazazi kila muhula.
ii. Kushirikiana na walimu na walezi kufuatilia na kuthibiti mwenendo na tabia ya mwanaye kwa kutoa maonyo na makaripio kwa wakati muafaka kwa kadri atakavyotakiwa au kuelekezwa na uongozi wa shule.

iii. Kushirikiana na walimu kufuatilia taaluma ya mwanae kwa kumpa mahitaji muhimu na mazingira salama ya kumwezesha kusoma kwa utulivu, kutoa karipio endapo maendeleo ya kitaaluma ya mtoto sio mazuri pamoja na kushiriki kubuni na kutekeleza mbinu bora za kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wote.

iv. Kuhakikisha mwanaye anapata malezi bora wakati wote awapo nyumbani kwa kuthibiti tabia ya uvivu na uzururaji inayosababisha wanafunzi kujiingiza katika makundi rika na hatimaye kuwasababishia kuiga tabia mbaya na kujiingiza katika mazingira hatarishi.

v. Kupata ripoti ya maendeleo ya Taaluma ya mtoto wake kwa wakati muafaka, kuhoji maendeleo duni ya mtoto wake na kupongeza walezi na walimu kwa maendeleo mazuri ya mtoto wake.

Mzazi ambaye hatatimiza wajibu wake ipasavyo atasababisha matatizo na usumbufu kwake na mwanaye kwani mwanafunzi atarudishwa nyumbani hadi hapo mzazi atakapoonesha ushirikiano wa dhati wa kumlea mtoto wake. Hivyo mzazi timiza wajibu wako kwa wakati bila kusukumwa kwa faida yako, ya mwanao na ya taifa zima.

## 4. TARATIBU NA KANUNI ZA KILA SIKU

Taratibuna kanuni hizi zifuatwe na kila mwanafunzi bila kusita na kwa wakati wote awapo shuleni. Kukiukwa kwa taratibu na kanuni hizi kutamsababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali ikiwemo kurudishwa nyumbani ili kukaa chini ya uangalizi wa mzazi kwa kipindi kisichopungua majuma matatu hadi miezi miwili wakati masomo yanaendelea ili kumrejesha katika mwelekeo unaotakiwa

i. Mwanafunzi avae sare za shule wakati wote wa siku za masomo na siku za ibada. Baada ya masomo na siku za jumamosi na jumapili mwanafunzi atavaa sare ya baada ya masomo (*home dress*).

ii. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa kandambili au viatu vya aina nyingine wakati akiwa katika sare rasmi ya shule tofauti na viatu alivyoagizwa.

iii. Mwanafunzi anatakiwa kuonekana katika hali ya kawaida na nadhifu. Hivyo mapambo yeyote kama vile bangili, hereni na mikufu hayaruhusiwi shuleni.

iv. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka au kuwa na nywele ndefu. Hivyo kila mwanafunzi afike shuleni na vifaa vya kunyolea nywele. Ruhusa haitatolewa kwenda kunyoa nje ya shule.

v. Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya shule bila ruhusa iliyoidhinishwa na Mkuu wa shule au Makamu Mkuu wa shule pamoja na Mwalimu wa Zamu na kuthibitishwa na Mwalimu wa darasa.

vi. Ni marufuku kabisa mwanafunzi **kuingia nyumba ya mtumishi** yeyote kwa sababu yeyote ile mchana au usiku.

vii. Ikiwa mwanafunzi ana matatizo ya nidhamu, ya kifamilia au ugonjwa, ni mzazi **pekee** ambaye picha yake iko katika maelezo ya mwanafunzi atakayewajibika kufika shuleni binafsi kumchukua, kusikiliza na kujadiliana na walimu kuhusu nidhamu au ugonjwa wa mwanaye. Mtu mwingine yeyote hatakabidhiwa wala kujadili matatizo ya mtoto asiye wake.

viii. Kila mwanafunzi anatakiwa kulala katika kitanda na bweni alilopangiwa muda wote awapo shuleni. Mwanafunzi kuhama bweni na kulala wawili ni kosa kubwa na ataadhibiwa vikali akibainika.

ix. Vyakula na milo yote iliwe katika bwalo la chakula na vifaa vya chakula vitunzwe katika makabati yaliyowekwa bwaloni.

x. Kila mwanafunzi anatakiwa kupata mlo wake katika meza yake aliyopangiwa na atawajibika kuisafisha baada ya kila mlo kwa utaratibu waliojiwekea.

xi. Jikoni ni mahali pa kutengeneza chakula hivyo panatakiwa kuwa safi wakati wote hivyo wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni bila sababu ya msingi.

xii. Vifaa vyote vya umeme na elektroniki kama vile redio, pasi, walk-man, heater simu na kamera haviruhusiwi kwa mwanafunzi awapo shuleni.

xiii. Manukato makali (*perfumes)* hayaruhusiwi kwa wanafunzi kwani harufu kali za manukato haya huwadhuru wanafunzi wengine kwa kuwaletea magonjwa ya mapafu kama vile pumu na kuwasababisha kukatisha masomo mara kwa mara kuhudhuria matibabu.

xiv. Mwanafunzi atakayelazimika kulala kwa ajili ya ugonjwa, ni lazima apate uthibitisho wa daktari kutoka katika hospitali inayotambulika na serikali.

xv. Mwanafunzi atakayeugua akiwa darasani na kuhitaji kwenda kupata matibabu katika zahanati ya shule anatakiwa apatiwe kibali toka kwa Mwalimu wa somo au Mwalimu wa darasa.

xvi. Wageni hawaruhusiwi kuonana na mwanafunzi wakati wa masomo. Mzazi anayehitaji kutoa mahitaji yeyote kwa mwanaye atapokelewa na mlinzi ambaye atawasilisha kwa Mwalimu wa zamu. Mwalimu wa zamu kwa utaratibu maalumu atampatia mwanafunzi. Mzazi hakikisha kifurushi au fedha ulizomletea mwanao zimesajiliwa katika kitabu maalumu na umetia saini kuepuka usumbufu.

xvii. Mwanafunzi atakayeripoti shuleni baada ya saa 10:00 jioni aidha wakati wa kufungua shule au apewapo ruhusa ya kwenda nje ya shule kwa sababu yeyote ile **ATARUDISHWA NYUMBANI** na atalazimika kufika shuleni na mzazi/mlezi kwa ajili ya kutoa maelezo ya sababu za kuchelewa kuripoti shuleni. Hatua zaidi zitachukuliwa endapo maelezo ya mzazi/mlezi hayataridhisha.

5. **MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhurua masomo kwa zaidi yasiku 90 bila taarifa/ utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezina jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi kumpigamwalimu au na mtu ye yote yule.
vi. Kusuka / kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga nywele/kucha.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara bangi/ Ugoro.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule bila idhini.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

## AHADI YA MZAZI

Mimi ……………………………………… Mzazi/mlezi wa …………………………………….. nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi. Aidha, nitalipa ada kwa wakati bila usumbufu.

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi …………………………………………… wa kidato cha ………………… nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na mzazi wangu. Nimejadiliana naye na nimezielewa vizuri kabisa. Ninaahidi nitazifuata bila kusukumwa wala manung'uniko na ninakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule endapo nitakiuka mojowapo ya sheria na taratibu hizi. **Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.**

Saini ya mzazi………………………………. Tarehe …………………………..

Saini ya mwanafunzi ……………………………. Tarehe………………………..

Ni imani yangu kuwa utafuata taratibu hizi ili uweze kujifunza kwa bidii kwa mafanikio yaliyo bora.

**Ninakutakia kila la kheri na karibu sana Machame Sekondari!**

……….................

**A.F. MASSAWE.**

**MKUU WA SHULE.**

*Machame Girls' Secondary School*
*P. O. Box 3043, Moshi.Mobile 0754349771. Fax 0272756897*

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Mmi …………………………………………………… nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa katika shule ya Sekondari ya Wasichana Machame. Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sheria na taratibu zote za shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, ya familia yangu nafaida ya taifa kwa ujumla. Ninaahidi kuripoti shuleni siku iliyopangwa bila kuchelewa.

Anuani ya kudumu ya mzazi/mlezi

……………………………………………….

………………………………………………

………………………………………………

……………………………………………..

Saini ya mwanafunzi………………………….

Saini ya mzazi…………………………….

Taerehe ……………………………….

## MACHAME SEKONDARI – SARE YA SHULE



HIJABU



KIATU



**SKETI MBELE**

ZIPU



**SKETI NYUMA**



SWETA MIKONO MIFUPI



SWETA MIKONO MIREFU



**GAUNI CHINI LIWE SOLO**

NB: Kwa maelezo zaidi/Changamoto wasiliana na uongozi wa shule

MACHAME SEKONDARI
ORODHA YA VITABU

GEOGRAPHY BOOKS.

1. Geography An Integrated Approach By David Waugh.
2. Human and Economic Geography. By Goh Cheug Leong, Gilliam C. Morgaw
3. Physical Geology Fourteenth Edition. By Plummer Carlson, Hammerslay
4. Principle of Physical Geography. By F.J Monkhouse
5. Practical Geography for Africa. By John M Prichard
6. Geography for secondary schools Form Five. By Tanzania Institute of Education.
7. Research methodology, Methods and Techniques. By C. R. Cothari.

ECONOMICS BOOKS
1. Modern Economics. By Robert Mudida
2. Modern Economics Theory. By Dr Dewett

ENGLISH BOOKS
1. The Beautiful ones are not yet Born. By Ayi kwei Armah
2. I will marry when I want. Ngugi wa Thiong'o and Ngugi wa Miriri
3. Betrayal in the city. By Francis Imbuga
4. Lwanda Magere. By Okoit Omtatah
5. A season of waiting. By David Omowale.
6. Oxford (2014) Advanced English Language form Five and six.
7. TIE (2016). English Language for Secondary school s. Language and Language use. Form Five and six. By Tanzania Institute of Education.

KISWAHILI BOOKS
1. Mwansoko, H na Wenzake (2006). Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu.
2. Nkwera, F (2003) Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo.
3. Msokila M (1992) Historia na Matumizi ya kiswahili
4. Mulokozi M (1996) Fasihi ya Kiswahili
5. Nkwera F (1978) Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo
6. Mutembei,A (2006) "Nadharia ya Fasihi simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia"
7. Oxford University Press – Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

AGRICULTURE BOOKS.
1. Sibuga, K. K and Isengwa, I.P (1986). Outlines of soil science:
2. Ngugi, D. N *et al,* (1990). East African Agriculture third Edition.
3. McDonald, P *et al* (1973). Animal Nutrition second Edition.
4. Sibuga K.K *et al* (2004). Principles and practices of livestock and crop production
5. Dihenga, H.O *et al* (1989) Introduction to Agromechanics Mzumbe Projects
6. Sibug, K.K Basic Agricultural Economics .
7. Lupatu, M.A An Introductory to Agricultural Economics
8. Certificate of Agriculture By Nyangom and Konyango.

BIOLOGY BOOKS
1. Biological science Third Edition. By Taylor G (1997).
2. Understanding Biology for Advanced level Third Edition. By Glenn T and Susan T (1995)
3. Advanced Level Biology Text Books for Form Five and Six By Ernest K (2009)

MATHEMATICS BOOKS

1. Advanced level pure mathematics fourth Edition By C.J. Tranter.
2. Pure Mathematics 1 By J.K Backhouse et al
3. Pue Mathematics 2 By J.K Backhouse et al
4. Understanding pure mathematics By A.J. Sadler and D.W.S Thorning
5. Engineering mathematics for B.E, A.M I. E ( Diploma & Non Diploma Stream) By S. Chand

HISTORY BOOKS

1. Essentials in Advanced Level History Paper Two. By Saleh Yassin.
2. History For Secondary Schools Form Six. By Tanzania Institute of Education.
3. A History of Modern Europe 1789 to 1981. Seventh Edition. By H. L . Peacock.
4. How Europe underdeveloped Africa. By. Walter Rodney.

CHEMISTRY BOOKS

1. Burns, R (1999). Fundamentals of Chemistry Third Edition, Prentrice Hall, Inc United
2. Jain S, (2005). Conceptual Chemistry for class XII, S. Chand & Company Pvt.Lt.New Delhi.
3. Ramsden E, (2000). A-Level Chemistry Fourth Edition, Nelson Thornes (Publishers) Ltd United Kingdom.
4. Melcafe D et all (2002). Modern Chemistry, Holt Rinehart and William, U.S.A.
5. T.I.E, (1995). Advanced Level Inorganic Chemistry Part I and II, Dar-es-salaam University Press. Dar-es-salaam.
6. Abdullah A, et all (1986). Organic Chemistry Part A and B, Tanznia Publishing House. Dar-es-salaam.

MATHEMATICS BOOKS

1. Advanced level pure mathematics fourth Edition By C.J. Tranter.
2. Pure Mathematics 1 By J.K Backhouse et al
3. Pue Mathematics 2 By J.K Backhouse et al
4. Understanding pure mathematics By A.J. Sadler and D.W.S Thorning

Engineering mathematics for B.E, A.M I. E ( Diploma & Non Diploma Stream) By S. Chand